**AckySHINE.com**

# Kupasuka kwa kondomu

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kupasuka kwa kondomu mara nyingi kunasababishwa na kondomu kutowekwa vizuri uumeni. Ni muhimu sana kutoa hewa ndani ya kondomu wakati wa kuvalisha uume. Kwa sababu ile hewa ndani ya kondomu inaweza ikasababisha kondomu kupasuka wakati wa kujamiiana. Vilevile siyo vizuri kupaka mafuta kama vaselini juu ya kondomu ili kurahisisha kitendo cha kuingiliana. Mafuta kama vaseline yanadhoofisha uimara wa kondomu na yanarahisisha kondomu kupasuka. Mafuta haya yanayowekwa kwenye pakiti ya kondomu yanahifadhi uimara wa kondomu, na ni aina maalumu ya mafuta. Ni muhimu kukumbuka kwamba mwanaume akivaa kondomu vizuri jinsi tulivyoeleza awali, uwezekano wa kondomu kupasuka ni mdogo sana.